OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

# OAG

# WIKI HII

*KWENYE*

# MAGAZETI

*NA*

MITANDAONI

# Wataka sera, sheria ulinzi wa mtoto iboreshwe

BARAZA la ulinzi wa mtoto wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma limeitaka serikali kushirikiana na wadau mbalimbali kuboresha sera na sheria ya ulinzi wa watoto ikiwamo sheria ya ndoa inayoruhusu mtoto mwenye umri wa miaka 14 kuolewa ili kutokomeza ukatili dhidi yao.

Wito huo ulitolea na mwenyekiti wa baraza hilo, Anthony Mlewa wakati wa mkutano wa baraza hilo uliofanyika katika kijiji cha Kawawa, kata ya Msanga wilayani Chamwino ulioandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Actionaid Tanzania yenye kauli mbiu "Elimu jumuishi kwa watoto izingatie maarifa, maadili na stadi za kazi".

Mlewa alisema ili kudhibiti ukatili unaoendelea dhidi ya watoto jitihada za wadau wote na serikali ni muhimu kwa maendeleo endelevu.

Mbali na hayo baraza limewaomba wanajamii kutoa ushirikiano kutoa taarifa dhidi ya ukatili kwa watoto.

Alibainisha kuwa miongoni mwa changamoto inazowakabili ni ushirikishwaji duni kwenye masuala mbalimbali yanayohusu watoto na maamuzi, ukiukwaji wa haki za watoto na uhaba wa miundombinu shuleni na kutaka iboreshwe.

"Mimba za utotoni, ndoa za utotoni, vipigo vilivyopitiliza bado ni tatizo, pale penye haki wazazi wana wajibu wa kuhakikisha ulinzi wa mtoto ni kipaumbele sio ombi, lakini pia wazazi wanawajibika kwenye masuala ya maadili kwa watoto,'' alisema.

Naye Mrakibu Msaidizi wa Polisi Yusuph Abdallah alisema kwa mujibu wa takwimu za wilaya ya Chamwino za Oktoba 2023 hadi Juni 2024 kesi za ukatili zilizoripotiwa kituo cha polisi Chamwino zilikuwa 118 kati ya hizo wanaume 109, wanawake tisa, watoto 26 ,kesi 88 zipo mahakamani, 32 zimeshawatia hatiani, miongoni mwa kesi hizo ni pamoja na ubakaji, ukeketaji na vipigo.

"Ulezi wa watoto unategemea pande kuu tatu, wazazi, walimu na wanajamii, wazazi tuwe karibu na watoto ili kujua mahitaji yao". Abdallah aliwataka wazazi kutoa taarifa kwa dawati la jinsia endapo watapata taarifa za ukiukwaji wa haki za binadamu.

Kwa upande wake Ofisa Ustawi wa Jamii wilayani Chamwino, Obed Fredy aliwataka wazazi kuacha tabia ya kuwaachia watoto simu muda mrefu ili kupunguza mmomonyoko wa maadili.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wakulima Wadogo Wilaya ya Chamwino (JUWACHA) chini ya Shirika la Actionaid Tanzania, Janeth Nyamayahasi aliwataka wazazi kutenga muda kwa ajili ya malezi ya watoto.

SHERIA

# Masaibu ya kisheria ukiishi kama kimada

Daniel Mjema, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz



**Mwanza.** Gladness Mujinja, aliyeishi na Sospeter Makene kama mume na mke kwa miaka 17, amepoteza haki ya mgawanyo wa mali walizochuma kwa miaka 17 baada ya Mahakama kutamka ndoa yao ilikuwa batili, kwani aliishi kama kimada.

Hayo yamo katika hukumu ya Mahakama ya Rufani Tanzania katika rufaa iliyokatwa na Makene dhidi ya Gladness, akipinga mahakama za chini kumpa mgawanyo wa mali, licha ya kutamka kuwa ndoa ilikuwa batili kisheria.

Hukumu hiyo ilitolewa Ijumaa ya Julai 12, mwaka huu na Mahakama ya Rufani iliyoketi Mwanza mbele ya jopo la majaji watatu ambayo ilibatilisha amri za Mahakama za chini juu ya mgawanyo wa mali na haki za kuishi na watoto wao watano waliowazaa.

Hukumu ya majaji--- Lugano Mwandambo, Lilian Mashaka na Gerson Mdemu, ilikubaliana na Mahakama za chini katika uamuzi kuwa wawili hao hawakuwa na ndoa halali, licha ya kuishi pamoja kwa miaka 17.

Katika maelezo ya rufaa, licha ya Mahakama kutamka ndoa ni batili, bado ilienda mbali na kutumia busara kugawa mali.

### Ndoa ilivyogonga mwamba

Maelezo yaliyotokana na mwenendo wa shauri hilo katika Mahakama ya Wilaya ya Nyamagana na Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza, Gladness na Makene waliishi pamoja kwa miaka 17 kati ya mwaka 1991 hadi mwaka 2014.

Januari 7, 1996 walijaribu kufunga ndoa ya kikristo ambayo ingefanya itambuliwe na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, lakini ilishindikana kanisani.

Ilibainika Gladness alikuwa na ndoa ya kimila na mwanamume mwingine aliyejitokeza kupinga ndoa hiyo isifungwe katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bunda mkoani Mara.

Wawili hao waliendelea na maisha kama kawaida hadi mwaka 2013, Gladness alipofungua maombi ya talaka katika Mahakama ya Wilaya ya Bunda, akidai kufanyiwa ukatili

> "Ilikuwa ni makosa kwa mahakama zote mbili kusikiliza na kutoa uamuzi wa nafuu aliyostahili Gladness wakati hiyo inatolewa tu pale kunapokuwa na talaka. Kwa vile hakuna sheria ya mgawanyo wa mali kwa kimada, busara haikuwa na nafasi."
>
> Hukumu

hakukubaliana kwamba kuishi kwao kulifanya uwepo wa ndoa kutokana na Gladness kuwa na ndoa na mwanamume mwingine. Alieleza hakuna mali walizochuma pamoja na kwamba Gladness hastahili kupewa haki ya kutunza watoto ambao alimtelekezea.

### Ndoa ilivyovunjwa, mgawanyo wa mali

Baada ya kusikiliza pande zote mbili, Mahakama iliona ushahidi wa Gladness ulithibitisha kuwapo ndoa ya kimila kati yake na mwanamume mwingine, kabla ya kuamua kuishi na Makene kwa miaka 17.

Mahakama ikatamka ni kweli wawili hao waliishi pamoja, lakini ikasema ndoa ilikuwa batili, kwani uhusiano wake na Makene ulikuwa wa mtu na kimada, haukuwa ndoa kwa mujibu wa sheria.

Mahakama iligawa mali walizochuma, Gladness akapewa ng'ombe watano na kiwanja kilichopo eneo la Nyasaka, lakini ikampa Makene haki ya kuishi na watoto kutokana na Gladness kuwatelekeza.

Makene hakuridhika na uamuzi huo, akakata rufaa Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza. Rufaa ilisikilizwa na Jaji Lameck Mlacha aliyetoa hukumu Septemba 21, 2016 akisema hapakuwa na ndoa halali.

Mahakama ya Rufani ilisema Jaji Mlacha aliona Gladness hakuwa na uwezo wa kuolewa na mwanamume mwingine kutokana na kuwa na ndoa ambayo haikuwa imevunjwa.

"Mahakama ya kwanza ya rufaa iliona kwa vile kulikuwa hakuna ndoa halali, hivyo talaka isingeweza kutolewa wala mgawanyo wa mali ambayo ilikuwa inadaiwa walikuwa wamechuma pamoja," inaeleza hukumu ya Mahakama ya Rufani

na mtoto mmoja na ikampa nyumba iliyopo Bunda, kiwanj po Kiseke na ng'ombe watano.

Mahakama Kuu pia ikaam ness apate asilimia 40 ya m mauzo ya kiwanja kilichopo kikiwa na mashine ya kusaga n 40 ya fedha zilizopo Benki z CRDB.

### Mabishano Mahakama ya Ruf

Makene hakuridhishwa n ya Mahakama Kuu Kanda ya akakata rufaa Mahakama Tanzania akiwa na hoja mbil mahakama za chini kukosea shahada ya bodi ya usuluhish

Alidai Mahakama ilikose kusikiliza ombi la talaka bila k hoja gani zinatakiwa kufanyi na Mahakama iliyolisikiliza aliridhishwa na hukumu ya Kuu, hivyo hakukata rufaa.

Wakili Constantine Mutal emwakilisha Makene alijeng Mahakama haikuwa sahih ombi la talaka kwa kuwa ha ambatanishwa na cheti kut Usuluhishi inayotambulika k

Akadai cheti hicho hakikutolewa kortini kama kielelezo, hivyo akaiomba Mahakama ya Rufani itumie mamlaka yake kubatilisha mwenendo wa shauri hilo kwa kuwa ulikuwa batili, ingawa hakunukuu msimamo wowote wa sheria.

Wakili Julius Mushobozi, aliyemtetea Gladness alipinga hoja hizo na kueleza miibu

TAARIFA ZAIDI

> Kutokana na uchambuzi huo, majaji walisema wanatumia mamlaka waliyopewa kupitia kifungu 4(2) cha mamlaka ya rufaa kurekebisha uharamu wa kisheria ullofanywa na Mahakama zote mbili.
>
> Hivyo, Mahakama ya Rufani imeamuru kubatilishwa kwa amri ya mgawanyo wa mali uliofanywa na Mahakama hizo na amri ya nani anastahili kuishi na watoto kwa vile zilikuwa amri batili, ila matamko yao kuwa ndoa ilikuwa batili yanasimama kama ilivyokuwa.

cha Sheria ya Ndoa, hivyo hakuwa na haja ya kuwasilisha tena cheti hicho kama kielelezo kortini.

Katika hukumu, majaji waliona mwenendo wa kesi haukuwa na tatizo, kwani Mahakama ya Wilaya Nyamagana ilisikiliza na kutamka kuwa hapakuwa na ndoa halali baina ya wawili hao, msimamo ambao ulichukuliwa pia na Mahakama Kuu.

### Uhalali mgawanyo wa mali

Katika hukumu, Mahakama ya Rufani ilisema baada ya Mahakama ya Wilaya ya Nyamagana kutamka hapakuwa na ndoa halali, ilipaswa iishie hapo na kuyatupa maombi ya talaka na haikupaswa kujielekeza kugawa mali.

Majaji walisema Jaji Mlacha ambaye ndiye ilikuwa ngazi ya kwanza ya rufaa, alifahamu uwapo wa kifungu cha sheria kinachosema hakuna amri ya mgawanyo wa mali inayoweza kutolewa pasipokuwa na talaka au ndoa halali.

"Hata hivyo, licha ya kubaini kuwa sheria haina kifungu kinachosimamia mgawanyo wa mali kutokana na kuvunjika kwa mahusiano ya masuria (kimada) kama ilivyo katika shauri hili, bado ilitoa amri ya mgawanyo wa mali," inaeleza hukumu.

"Mahakama (Kuu) iliendelea kutoa amri ya mgawanyo wa mali na haki ya kuishi na watoto ikiegemea busara kuhalalisha kwenda na njia hiyo.

"Mamlaka ya Mahakama kutoa haki imepewa kupitia Ibara ya 107A na 107B ya Katiba," wanaeleza majaji katika hukumu.

Akinukuu Ibara hiyo, inasema "Katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, Mahakama zote zitakuwa huru na kuzingatia tu masharti ya Katiba na sheria za nchi," hivyo wakasema sheria inataka kuvunjwa kwa ndoa halali tu.

"Baada ya Mahakama kutamka kuwa kulikuwa hakuna ndoa ya mume na mke, ilitakiwa kuishia hapo na kuyatupa maombi ya talaka. Kwa vile haikufanya hivyo, ngazi ya kwanza ya rufaa

# 'Maofisa ugani wasimamie sheria kukabili sumukuvu'

Na Sifa Lubasi

MAOFISA ugani na watendaji wa kata katika Halmashauri ya Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, wametakiwa kusimamia sheria ndogo ya kukabili sumukuvu ili wawe na uelewa wa pamoja.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Zaina Mlawa alisema hayo akifungua mafunzo chini ya Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu (TANIPAC) unaotekelezwa na Wizara ya Kilimo.

Alisema ni muhimu kwa maofisa kujua sheria ndogo ya kukabiliana na sumukuvu ili kwenda kuisimamia katika maeneo yao.

Alisema mwaka huu Wilaya ya Bahi imezalisha chakula cha kutosha.

"Mwaka huu tunajivunia, tunaweza tusilalamike njaa kwa sababu takwimu nilizonazo, kile kipimo cha ukusanyaji wa mazao ambacho tulitakiwa kuwa nacho tumepita yaani tuna ziada," alisema.

Aliongeza, "tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa msimu uliopita katika Halmashauri ya Wilaya ya Bahi tuliweza kuletewa mbegu za bure kwa ajili ya kusaidia wananchi kulima, tulileteww tani ya mtama mweupe na mbegu za alizeti, hivyo hatukuwa na sababu ya kusema tulikuwa na njaa."

Kwa upande wake, Ofisa Kilimo Mkuu Wizara ya Kilimo, Margaret Natai alisema kutokana na madhara yanayotokana na vimelea vya sumukuvu, serikali iliamua kuanzisha mradi huo na kuanza utekelezaji mara moja.

Alisema wameandaa sheria ndogo kwa ajili ya kupambana na sumukuvu.

Alisema chanzo ni wananchi kutokuwa na uelewa juu ya namna bora ya kutunza mazao yao kuanzia shambani mpaka yanapofika sehemu ya kuyahifadhi.

Alisema serikali ikaona kuna haja ya kutoa elimu kwa wakulima wajue njia bora za kutunza mazao yao pamoja na kujua njia bora za kilimo.

Alisema sumu hazionekani kwa macho, hazina harufu, ladha wala rangi.

"Lakini kuvu wanaozalisha sumukuvu wanaweza kuwa na rangi kama vile kijani, kijivu, njano chafu au machungwa," alisema.

Ofisa mradi wa kudhibiti sumukuvu Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Hamis Mfuko alisema wao ni kati ya wilaya 18 zinazotekeleza mradi wa kudhibiti tatizo hilo.

Mkuu wa kitengo cha Sheria Bahi, Martha Chamwela alitoa wito kwa watendaji wa kata na maofisa ugani kusimamia sheria zaidi kuanzia hatua za awali kwa wakulima.

nda nguvukazi ya Taifa inavyotekeleza majukumu yake ya msingi

# Dk. Feleshi akoshwa utendaji makini wa OSHA

**NA MWANDISHI WETU**

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi, ameupongeza Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi nchini.

Dk. Feleshi alitoa pongezi hizo jijini Dar es Salaam hivi karibuni alipotembelea banda la OSHA katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba).

"Naupongeza Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi nchini,"alisema.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema wakala huo wenye dhamana ya kulinda nguvukazi ya Taifa inavyotekeleza majukumu yake ya msingi.

"Katika kutimiza wajibu wetu wa kusimamia utekelezaji wa Sheria Na. 5 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003, tunaanza kwa kutambua maeneo ya kazi kwa kuyasajili na kuweka utaratibu mzuri wa wataalamu kufika katika maeneo husika kwa kufanya ukaguzi wa mifumo ya usalama na afya na kushauri uboreshaji unaohitajika,"alisema.

Kuhusu mkakati unaotumika na OSHA kuyafikia maeneo yote ya kazi nchini, Dk. Feleshi alisema mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ndiyo nyenzo inayotumika kuyafikia maeneo ya kazi kiurahisi.

"Tunatumia mfumo wetu wa kieletroniki wa usimamizi wa taarifa za maeneo ya kazi ambao unatuwezesha kuwasiliana na wadau wetu kwa njia rahisi na haraka ambapo kupitia mfumo huo wadau wetu wapate huduma zetu mbali mbali ikiwemo kusajili sehemu za kazi wakiwa mahali popote, kuwasilisha taarifa za ajali, kujisajili kupata mafunzo na kuwasilisha taarifa za ajali zinazotokea mahali pa kazi," alisema.

Alitaja changamoto ambazo OSHA inakabiliana nazo ni uelewa mdogo wa masuala ya usalama na afya miongoni mwa wananchi pamoja kasi kubwa ya ukuaji wa teknolojia ya uzalishaji katika maeneo ya kazi ambayo huzalisha vihatarishi vipya kila mara.

SHERIA--

# Mahakama Kuu yaridhia Kitale kuishtaki TLS



Wakili, Steven Kitale (aliyesimama) akizungumza na mawakili wenzake wakati wa shauri la maombi ya mapitio ya kisheria dhidi ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), katika Mahakama Kuu kanda ya Mwanza. **Picha na Mgongo Kaitira**

**UAMUZI WA JAJI**

**Akisoma uamuzi, Jaji Matuma alisema Mahakama inakubaliana kuwa Kamati ya Uchaguzi wa TLS na upandishaji wa ada za wanachama kuhudhuria AGM ya 2024, kutoka Sh118,000 hadi Sh200,000, hazikupata baraka za wajumbe wote wa Baraza la Uongozi, hivyo uamuzi huo unakiuka misingi ya kisheria.**

**"Muombaji anasema kunyimwa nyaraka hizo kunamfanya aone mchakato wa uchaguzi umegubikwa na mapungufu ya kisheria na amethibitisha kesi inayohitaji ufafanuzi wa kimahakama na kisheria. Pia, uchaguzi ni mchakato wa kisheria na wasimamizi wa uchaguzi husika lazima wapatikane kwa kuzingatia miongozo ya kisheria," alisema Jaji Matuma.**

Mgongo Kaitira, Mwananchi
mkaitira@mwananchi.co.tz

**Mwanza**. Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza imetoa ruhusa kwa Wakili Steven Kitale kuwasilisha maombi ya mapitio ya kisheria dhidi ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kuhusu uhalali wa wajumbe wa kamati ya uchaguzi ya chama hicho.

Pia kufanya marejeo kuhusu TLS kupandisha ada za wanachama wake kuhudhuria Mkutano Mkuu wa mwaka misha mchakato wa uchaguzi mkuu wa chama hicho unaojumuisha shughuli za Kamati ya Uchaguzi na Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi, badala yake imemtaka mleta maombi kuwasilisha maombi ya mapitio ya kisheria kwanza.

Shauri hilo lililotawaliwa na upinzani wa hoja kutoka pande zote, lilisikilizwa juzi mbele ya Jaji Athuman Matuma kuanzia saa saba mchana na uamuzi kutolewa saa 2.30 usiku.

Katika shauri hilo, mleta maombi Kitale anawakilishwa

Upande wa wajibu maombi, ambao ni TLS, Mkurugenzi Mtendaji wa TLS, Baraza la Uongozi la TLS, na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) umewakilishwa na Wakili Mkuu, Lameck Merumba, mawakili Subira Mwandambo, David Shiratu na Hekima Mwapusi.

Mbele ya Jaji Matuma, wajibu maombi wakiwakilishwa na wakili Mwapusi walileta pingamizi wakiwa na hoja tano kwenye shauri la msingi la maombi ya mapitio ya kisheria.

Akisoma hoja hizo, Mwa-

unaolalamikiwa, kukosa uwezo wa kisheria, kiapo cha mleta maombi ni batili, maombi ni ya kipuuzi, ya kero na matumizi mabaya ya mchakato wa Mahakama.

"Maombi haya hayana msingi wa kisheria, bali ni hila na ghiliba za kisheria. Mleta maombi anazuia mkutano mkuu wa mwaka (AGM) kwa masilahi gani? Mkutano wa mwaka gani? Ya tarehe gani? Hajaeleza anazuia mchakato upi wa uchaguzi. Kwa hiyo tunaiomba Mahakama yako kutupilia mbali

Jaji Matuma alisema Mahakama imejiridhisha pasi na shaka kwamba hoja za mleta maombi zina nguvu na msingi kisheria wa kusimama na kusikilizwa.

"Baada ya kusikiliza hoja za pande zote, mawakili wa mleta maombi waliwasilisha hoja wakirejelea yaliyozungumzwa kwenye kiapo cha mleta maombi. Kwa mujibu wa nyaraka hizo, katika mkutano wa dharura wa 10 wa Baraza la Uongozi la TLS, liliainisha ada, lakini kwa namna ambayo haijawekwa bayana.

"Ni wazi kwamba muombaji, ambaye ana masilahi mapana kwenye jambo hili kama mjumbe wa Baraza la Uongozi, ana jukumu la kusimamia wajibu na uwajibikaji. Aliomba nyaraka zinazoidhinisha uteuzi wa Kamati ya Uchaguzi na Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi, lakini alinyimwa nyaraka hizo," alisema.

Akisoma uamuzi, Jaji Matuma alisema Mahakama inakubaliana kuwa Kamati ya Uchaguzi wa TLS na upandishaji wa ada za wanachama kuhudhuria AGM ya 2024, kutoka Sh118,000 hadi Sh200,000, hazikupata baraka za wajumbe wote wa Baraza la Uongozi, hivyo uamuzi huo unakiuka misingi ya kisheria.

"Muombaji anasema kunyimwa nyaraka hizo kunamfanya aone mchakato wa uchaguzi umegubikwa na mapungufu ya kisheria na amethibitisha kesi inayohitaji ufafanuzi wa kimahakama na kisheria. Pia, uchaguzi ni mchakato wa kisheria na wasimamizi wa uchaguzi husika lazima wapatikane kwa kuzingatia miongozo ya kisheria," alisema Jaji Matuma.

**Kitale aridhishwa**

Akizungumza kwa niaba ya mleta maombi (Kitale), Wakili Erick Mutta alisema mteja wake ameridhishwa na uamuzi uliotolewa na Mahakama, akiahidi kufungua

# MSLC benefits 478 during trade fair

By DATIVA MINJA

ACTING Director of Legal Aid Service in the Ministry of Constitution and Legal Affairs, Ms Ester Msambazi has said that a total of 478 Tanzanians have benefited from the Mama Samia Legal Aid Campaign (MSLAC) during the 48th Dar es Salaam International Trade Fair (DITF) exhibition which ended over the weekend.

The service provided included legal education, advice, preparation of legal documents, marriage and land disputes. She said 333 of beneficiaries were men and 145 were women.

"We have provided legal advice, connecting them with lawyers, helping them resolve their disputes in administrative ways, land disputes and legal education," she noted.

According to Ms Msambazi, the platform has provided an opportunity for her office to link the public to legal aid providers and the pool of lawyers.

Ms Msambazi said a total of 125 cases were registered among 30 were for land, eight marriages, 22 inheritances, six criminal, 16 claims, 16 employment, five childcare, one gender-based violence and 21 others.

"Many of them who visited our pavilion were seeking assistance in understanding some legal issues or getting advice on whether they have proper cause to file a case at the court of law, "said Ms Msambazi.

She said that the legal aid is provided by the ministry in collaboration with various stakeholders including eight lawyers from Tanganyika Law Society (TLS), two legal assistants and one student from Law school.

She said that the campaign team is well organised to assist with drafting all the legal papers free of charge.

Further she said since it was first launched last year the campaign has reached seven regions and attended over 490,000 people.

Details from the campaign organisers indicate that at least 214,888 men and 200,392 women had benefited. This also includes 6,824 men and more than 340 women detained or serving in different penitentiaries.

Legal aid encompasses rights and legal protection for all individuals regardless of gender or circumstance. MSLAC says its goal is to assist individuals, helping them understand related laws and procedures. "It's not a gender issue."

MSLAC provides legal aid to men and women facing abuse by their partners, children deprived of basic rights by parents, guardians, or their community and disabled individuals experiencing mistreatment, along with counselling and training on protective laws.

Ms Msambazi said MSLAC offers legal aid and basic rights guidelines for prisoners, individuals in despair, the lonely, and those feeling disadvantaged by the legal system.

"Like I said, MSLAC also offers legal aid in marriage disputes, inheritance matters, governance, gender-based violence, child support and community-wide legal education."

To ensure accessibility, 256 organisations are registered to provide free legal aid services to citizens.

Mr Yunus Lingani, a resident of Dar wa Salaam said the campaign helped him get his rights. He said MSLAC has helped him to get his plot back in Mkuranga, Coast Region and that he is still following the case for another plot in the same area under the support of the Legal Aid Campaign.



# Mwabukusi hatua moja, mawakili 29 kumtetea

Hadija Jumanne, Mwanachi
hjumanne@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam imemruhusu Wakili Boniface Mwabukusi kufungua shauri la marejeo ya uamuzi uliomwengua kwenye orodha ya wagombea urais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS).

Hata hivyo, imekataa ombi la kusimamisha mchakato wa uchaguzi huo, ambao sasa utaendelea kama ulivyokuwa.

Umuzi huo ulitolewa jana na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Salma Maghimbi baada ya kupitia maombi ya Mwabukusi na hoja zilizotolewa na wajibu maombi ambao ni TLS.

Mwabukusi alifungua shauri hilo Julai 11, 2024 katika Mahakama Kuu ya Tanzania Masjala Ndogo ya Dar es Salaam.

Wakili huyo alikuwa miongoni mwa wagombea sita waliopitishwa na Kamati ya Uchaguzi ya TLS kugombea nafasi hiyo Juni 24, 2024.

Wagombea wengine waliopitishwa kuwania urais katika uchaguzi uliopangwa kufanyika Agosti 2, jijini Dodoma ni Ibrahim Bendera, Emmanuel Muga, Revocatus Kuuli, Paul Kaunda na Sweetbert Nkuba.

Hata hivyo, kwa sababu ya doa la kimaadili, Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi TLS ilimuengua Mwabukusi kwenye kinyang'anyiro hicho, kitendo anachokipinga.

Mwabukusi aliiomba Mahakama kutoa ruhusa ya kufanya marejeo, akidai Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi ya TLS imemuengua pasipo kumpa nafasi ya kusikilizwa.

Anadai kulikuwa na ukiukwaji wa haki za binadamu na haki ya asili kwa kutoa hukumu bila kumshirikisha.

Pia, aliomba zuio la mchakato wa uchaguzi wa TLS ngazi ya urais.

Akitoa uamuzi, Jaji Maghimbi alisema kusimamisha uchaguzi kwa nafasi ya urais Mahakama imeona hakuna sababu ya msingi ya kuweza kufanya hivyo na kwamba, baada ya kupewa ruhusa ana siku 14 za kufungua shauri la marejeo.

"Mleta maombi alikuja kwa ajili ya kuleta maombi ya kupata ruhusa ya kusajili marejeo na kuzuia uchaguzi katika nafasi ya urais, hivyo Mahakama imekuruhusu kufanya Judicial Review, kama jinsi ulivyoomba," amesema Jaji.



Wakili Boniface Mwabukusi (kushoto) akijadiliana jambo na Mwenyekiti wa Mawakili Vijana kutoka Chama Wanasheria Tanganyika (TLS,) Edward Heche katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam jana. **Picha na Hadija Jumanne**

## Mawakili 29 kumtetea

Mawakili 29 wa kujitegemea walijitokeza mahakamani kumtetea Mwabukusi katika shauri hilo, wakiongozwa na Mpare Mpoki, akisaidiana na Jebra Kambole, John Malya anayemwakilisha Pater Kibatala, Dickson Matata, Edward Heche na Ferdinand Makore.

Upande wa wajibu maombi ambao ni TLS wanawakilishwa na Wakili Steven Mwakiborwa na Hekima Mwasipu.

Awali, shauri hilo lilipoitwa mahakamani, Mpoki aliieleza Mahakama lilipangwa kutajwa na upande wa wajibu maombi wamekubali kuwa wamepokea nyaraka. Alisema mawakili wa kujitegemea wapatao 29 wakiongozwa na yeye watamtetea Mwabukusi.

Jaji Maghimbi baada ya kusikiliza hoja hizo, aliahirisha kwa muda shauri hilo hadi alipotoa uamuzi.

Jana, kesi ilipangwa kusikilizwa saa tatu asubuhi, lakini iliahirishwa hadi saa 6.20 mchana. Jaji Maghimbi alisikiliza hoja za pande zote na kisha kuahirisha kwa muda kwa ajili ya kwenda kuandika uamuzi ambao aliutoa saa 9:04 mchana.

# MITANDAONI

oagtanzania



oagtanzania



oagtanzania HABARI PICHA

Menejimenti ya  Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali leo tarehe 19 Julai 2024, imekutana na kufanya Kikao na Wakaguzi wa nje  kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kikao hicho kiliongozwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria Msaidizi Bw. Said Nzori, kimefanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa  Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilizoko Mtumba Jijini Dodoma.

OAG Tanzania
6m ·

HABARI PICHA

Menejimenti ya  Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali leo tarehe 19 Julai 2024, imekutana na kufanya Kikao na Wakaguzi wa nje  kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kikao hicho kiliongozwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria Msaidizi Bw. Said Nzori, kimefanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa  Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilizoko Mtumba Jijini Dodoma.

See translation









